Fasihi ya Kiswahili:
Urithi na Ubunifu wa Kisasa

▪ Dr. Mohamed Younes Khalifa Daw [*]   ▪ Saad bouazoum mehimd ali [**]

● Received: 11/ 10 / 2025.   ● Accepted : 03/ 12 /2025

■ **Ikisiri**

Fasihi simulizi ni fasihi inayotolewa au kusimuliwa kwa njia ya mdomo. Hii ni fasihi ya mwanzo kabisa katika historia ya mwanadamu. Fasihi hii ilianza pale tu mwanadamu alipoanza kufanya kazi akiwa na azma ya kuyatawala maisha yake. Nyimbo ni kipera cha mwanzo kabisa mwanadamu kukitumia. Nyimbo ziliimbwa kwa lengo la kuhamasisha utendaji kazi, kujiburudisha na hata kuonesha huzuni katika jamii.

Fasihi simulizi ina vipera vyake muhimu katika jamii. Taarab ikiwa ni kipera cha fasihi simulizi ina jukumu la kuelimisha, kuburudisha na kuhuzunisha kupitia mashairi yake.

● **Key words:Fasihi, Simulizi, Katika, Njia, Nyimbo**

■ **المستخلص:**

الأدب الشفهي هو الأدب الذي يُنقل أو يُروى شفهيًا. وهو أقدم أشكال الأدب في تاريخ البشرية. بدأ هذا الأدب عندما شرع الإنسان في العمل بهدف التحكم في حياته. تُعد الأغاني أقدم أشكال التعبير التي استخدمها الإنسان. كانت الأغاني تُغنى بهدف تحفيز العمل، والتسلية، وحتى التعبير عن الحزن في المجتمع.

للأدب الشفهي أدوار مهمة في المجتمع. فالطَرب، كونه أحد أشكال الأدب الشفهي، له دور في التثقيف والترفيه والتعبير عن الحزن من خلال قصائده.

الكلمات المفتاحية: الأدب، السرد، في، الطريق، الأغاني

* Associate Professor, Department of African Languages, Faculty of Languages, University of SebhaE-maiI:Moh.abouqrasah@sebhau.edu.ly

* * Assistant Professor, Department of Languages and African Studies – Faculty of Languages, University of SebhaE-maiI: aaad4144379@gmail.com

Sura ya kwanza

Utangulizi

Fasihi simulizi ni fasihi inayotolewa au kusimuliwa kwa njia ya mdomo. Hii ni fasihi ya mwanzo kabisa katika historia ya mwanadamu. Fasihi hii ilianza pale tu mwanadamu alipoanza kufanya kazi akiwa na azma ya kuyatawala maisha yake. Nyimbo ni kipera cha mwanzo kabisa mwanadamu kukitumia. Nyimbo ziliimbwa kwa lengo la kuhamasisha utendaji kazi, kujiburudisha na hata kuonesha huzuni katika jamii.

Fasihi simulizi ina vipera vyake muhimu katika jamii. Taarab ikiwa ni kipera cha fasihi simulizi ina jukumu la kuelimisha, kuburudisha na kuhuzunisha kupitia mashairi yake.

1.0 Usuli wa tatizo

Neno taarab limefasiriwa na wataalamu mbalimbali na kuweza kutoa maana zenye kukaribiana. Kwa mujibu wa Rais mstaafu wa Tanzania, Mzee Mwinyi, akinukuu kamusi ya Al-Maurid, anasema:

"Taarab ni furaha iliyokithiri, raha iliyoje, starehe, staladhi, tafrija, muziki, kuimba au kughani." (Khatib, 2014)

Pia, kwa mujibu wa kamusi ya Kiarabu na Kiingereza Al-Faraid al-Durriyya, neno lililonukuliwa na Khatib (2014), neno taarab linanyambulika na kuwa tariba, yatrib au taraba. Maneno yote hayo yanamaanisha furaha. Kamusi nyingine ya A Learner's Arabic-English Dictionary inaeleza kuwa neno:

"Taarab lina maana ya kutiwa hamasa, kuwa na furaha, kusherehekea karamu, kuimba au kupiga muziki." (Khatib, 2014)

Naye Andanega (2002) anasema kuwa:

"Neno taarab linahusiana na aina ya ngoma inayoitwa tarabu na pia na neno la Kurdu-Kihindi tarabu, maana yake ni furaha." (Andanega, 2002:109)

Kutokana na maana zote hizo, taarab ni hali ya upigaji muziki kwa furaha. Taarab hupigwa katika shughuli mbalimbali za kijamii ambapo watu huburudika kupitia mashairi yake. Hata hivyo, jambo la kushangaza ni kuwa

tafsiri zote hizo zinaelekeza taarab kimaana katika ramsa tu na kusahau kuwa taarab huweza kubeba dhamira za simanzi au hata tanzia. Zipo nyimbo nyingi ambazo mashairi yake hubeba hali ya jitihada, maafa au majonzi yanayowakumba wanadamu katika maisha yao ya kila siku. Taarab haimo katika ombwe, hivyo mashairi yake lazima yaguse maisha ya watu katika jamii.

Taarab ilipoanza Zanzibar katika kasri ya Sultani, nyimbo nyingi zilizoimbwa wakati huo zilikuwa za kumsifu na kumtukuza Sultani aliyekuwa madarakani. Nyimbo za kuomba dua juu ya mapenzi ya Sultani na Malkia wake, kumsifu Muumba na maumbile ya ulimwengu, pamoja na nyimbo za mikasa hazikukosa (Khatib, 2014).

1.1 Tamko la tatizo

[Marejeleo yote yamepangwa upya kwa mpangilio wa alfabeti na kuandikwa kwa mtindo mmoja wa kitaaluma kama ulivyokuwa awali bila kubadili chanzo chochote.]

Sura ya pili : mapitio ya maandiko

2.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha mapitio ya maandiko mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu chimbuko, historia, maendeleo, maudhui na fani ya muziki wa taarab, hususan taarab ya Zanzibar. Lengo ni kubainisha yale yaliyoandikwa tayari na kuonyesha pengo la utafiti ambalo kazi hii inalenga kuliziba.

2.1 Chimbuko la taarab zanzibar

Kila jambo au sanaa hutokea duniani huwa na asili na chanzo cha kuibuka kwake. Waandishi wengi wameandika vitabu, majarida na makala kuelezea chimbuko, historia na maendeleo ya taarab Zanzibar. Kati ya waandishi hao ni Khatib (2014) na Mgana (1991).

Khatib (2014) katika kitabu chake Taarab Zanzibar anaeleza kuwa taarab ilianza katika kipindi cha Sultan Seyyid Barghash (1870–1888). Sultan huyu alikuwa mtu aliyependa starehe na anasa, hivyo muziki wa taarab ukawa unapigwa katika kasri yake ya Beit-el-Ajaib kwa lengo la kumstarehesha.

Inaelezwa kuwa Sultan Seyyid Barghash aliagiza watu waliokuwa wajuzi wa muziki kutoka Misri kuja kumpigia muziki huo. Baadaye alimpeleka mtu

maalum huko Misri aliyeitwa Mohammed Ibrahim ili apate kufundishwa stadi za muziki wa taarab (Khatib, 2014:1–2). Aliporudi Zanzibar, Mohammed Ibrahim alikuwa tayari amejifunza kuimba na kutumia ala za taarab.

Inaaminika kuwa nyimbo za taarab wakati huo zilikuwa za Kiarabu kitupu. Kikundi maalum cha taarab cha Sultan kikaanzishwa, na sanaa hii iliendelea kumstarehesha Sultan na familia yake hata baada ya kifo chake.

Katika utawala wa Sultan Khalifa bin Haroub (1911–1960), taarab iliendelezwa na kupaliliwa zaidi kwa lengo la kumstarehesha Sultan na kumwondolea mawazo na machofu yaliyomkabili.

Baada ya kudidimia kwa mifumo ya kisultani, taarab iliendelea kukua na kuenea miongoni mwa wananchi wa kawaida. Vikundi binafsi vya taarab vilianzishwa mapema sana, ikiwemo Naad Akhwan Safaa (1905), Naad Shuub (1908) na nyingine nyingi (Khatib, 2014; Mgana, 1991).

Baadhi ya vikundi vilivyoanzishwa baadaye ni Royal Air Force (1945), Nuru-l-Uyunn (1945), Navy (1945), Banati (1945), Michenzani (1955), Miembeni (1957), Kwa Alamsha (1964), Culture (1964), Wardah el Baidha (1985), Mila na Utamaduni (1986), Polisi (1986), Jeshi (1989) na Bwawani Musical Club (1989) (Mgana, 1991).

Awali vikundi vyote vilifuata mtindo wa taarab asilia. Baadaye vikundi kama vile East African Melody, Tanzania One Theatre (TOT), Zanzibar Stars na Dar-es-Salaam Modern Taarab vilifuata mtindo wa taarab ya kisasa.

Mabadiliko makubwa yalijitokeza katika matumizi ya vyombo vya muziki na uchezaji wa jukwaani kutokana na kuanza kutumika kwa vyombo vya kielektroniki. Ala za asili kama vile udi, violin, dumbaki na daf zilianza kuachwa. Baadhi ya wataalamu wanaamini kuwa uasili na utamu wa taarab asilia umeanza kupotea kutokana na mabadiliko hayo.

2.2 Maandiko yahusuyo taarab

Muziki wa taarab umeenea kwa kasi kutokana na mahadhi na mashairi yake kugusa mioyo ya watu wengi. Wataalamu mbalimbali wamefanya tafiti zinazohusiana na maudhui, fani na mchango wa taarab katika jamii.

Alawiya (2007) alifanya utafiti juu ya Nyimbo za mafumbo za taarab zinavyochangia kudumisha maadili ya jamii ya Wazanzibari. Alibaini kuwa

nyimbo za taarab zimechangia sana katika kukuza maadili ya jamii na kulinda mila na desturi za Wazanzibari.

Saleh (1980) katika utafiti wake juu ya Maudhui ya nyimbo za taarab za Unguja alieleza kuwa lugha ni kipengele muhimu kinachosaidia jamii kupata maudhui ya nyimbo kwa urahisi. Aliongeza kuwa baadhi ya nyimbo hutumia lugha nzito yenye mafumbo ambayo si rahisi kueleweka kwa haraka.

Thabit (2007) katika utafiti wake Nyimbo za taarab katika jamii ya Zanzibar alibaini kuwa maudhui ya nyimbo za taarab yana umuhimu mkubwa katika kujenga malezi na maadili mema katika jamii.

Alhabib (2012) katika utafiti wake juu ya matumizi ya lugha katika nyimbo za taarab alieleza kuwa lugha ya taarab imejaa mafumbo, sitiari, ishara na taswira zinazovutia wasikilizaji.

Broughton na wenzake (2000) kama walivyonukuliwa na Khamis (2012) walidai kuwa kimaudhui nyimbo za taarab hulenga zaidi mapenzi na hutumia fani ya mafumbo na sitiari.

Mzee (2013) alifanya utafiti juu ya Maudhui katika nyimbo za taarab za Bi. Shakila. Alibaini kuwa matumizi ya lugha yana mchango mkubwa katika kuibua dhamira mbalimbali na kufikisha ujumbe kwa jamii.

Hamisi (2012) alifanya utafiti juu ya Matumizi ya taswira na mafumbo katika nyimbo za mapenzi za taarab asilia. Alieleza kuwa taarab ya asilia imelenga kuadilisha jamii kwa kutumia lugha yenye staha.

2.3 Pengo la utafiti

Mapitio ya maandiko yanaonesha kuwa watafiti wengi wamejadili taarab katika vipengele vya chimbuko, maudhui, fani, taswira na matumizi ya lugha. Hata hivyo, hakuna utafiti uliobainika kujikita mahsusi katika kuchunguza nyimbo za huzuni katika taarab na dhamira zake.

Kwa hiyo, utafiti huu unakusudia kuziba pengo hilo kwa kuchunguza dhamira na sababu za kutungwa kwa nyimbo za huzuni katika taarab, hususan nyimbo zilizoimbwa na Fatma Issa.

Sura ya tatu : uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo

3.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha, kuchambua na kujadili data zilizokusanywa kuhusu dhamira na sababu za kutungwa kwa nyimbo za huzuni katika muziki wa taarab. Uchambuzi umeongozwa na nadharia ya uhalisia na maswali ya utafiti.

3.1 Dhana ya huzuni

Huzuni kwa mwanadamu ni hali ya masikitiko, majonzi, jitimai au simanzi ambayo mtu huipata ndani ya nafsi yake. Huzuni huwa na visababishi kadhaa katika jamii kama vile misiba, maradhi, usaliti na kadhalika. Dhana ya huzuni si ngeni masikioni mwa walio wengi kwani hujitokeza mara kwa mara katika maisha halisi ya kila siku. Mwanadamu hupatwa na huzuni kupitia mambo mbalimbali yanayotendwa. Huzuni humfika mtu yeyote lakini kila mmoja huwa na namna yake ya kuipokea au kuikabili. Wapo wanaonyamaza, wengine husononeka sana na kuathirika kisaikolojia, na wengine wenye vipaji kama washairi na waimbaji huiweka huzuni yao hadharani kupitia sanaa.

3.2 Sababu za kutunga nyimbo za huzuni

3.2.1 Usaliti

Usaliti lina asili ya neno salata lenye maana ya usaliti au ujeuri. Katika muktadha wa mapenzi, usaliti ni tendo la kumdanganya mpenzi. Ni hali ya mtu kutojiaminisha kwa mwenziwe au kumuendea kinyume juu ya mambo ambayo hayapaswi kufanyiana katika maisha ya kawaida.

3.2.2 Usaliti wa mume na mke

Usaliti wa mume na mke si geni katika jamii zetu. Mara nyingi hujitokeza pale mmoja wa wanandoa anapovunja uaminifu kwa kufanya tendo la ndoa nje ya ndoa. Hali hii hupelekea migogoro, mifarakano na hata kuvunjika kwa ndoa.

Mshairi na mwimbaji aliyefikwa na masaibu hayo anatunga wimbo wa Nenda Utakako. Katika beti ya kwanza anamruhusu mpenzi wake aende atakako, japokuwa anakiri bado anampenda. Anaimba:

Nenda nenda utakapo nenda

Nenda hujazuiliwa

Japo kuwa nakupenda

Kwa hilo sitoumbiwa

Katu mimi sitojali zako inda

Ulichoweka chukua

Kwapani sitokuganda

Kwako nikajizuzua

3.2.3 Usaliti wa rafiki au ndugu

Usaliti kati ya rafiki, ndugu au jamaa hujitokeza pale mtu wa karibu anapofanya vitendo visivyostahiki kufanyiwa rafiki au ndugu. Utafiti umebaini kuwa usaliti wa aina hii husababisha huzuni kubwa na kuvunjika kwa mahusiano

3.3 Msiba

Msiba ni hali ya mtu kuondokewa na mwenza au mtu wake wa karibu kwa kusafiri au kufariki dunia. Hali hii humjaza mwanadamu huzuni na simanzi kubwa.

Wimbo wa Adui Kiumbe ulioimbwa na Fatma Issa unaonesha masikitiko hayo kwa binadamu wenzake.

3.4 Maliwazo na ufariji

Imebainika kuwa wasikilizaji wanapozisikiliza nyimbo za taarab asilia zenye maudhui ya huzuni nao huguswa hisia nzito kutokana na kukumbuka hali zilizowakumba wao binafsi.

Wimbo wa Haya Maumbile Yangu uliotungwa na kuimbwa na Fatma Issa huwagusa watu wengi kutokana na tungo ya mashairi yake na mlio wa vinanda vyake. Beti zifuatazo zinaonesha hisia hizo:

Ubinafsi na choyo

Nyoyoni vyawasumbua

Kutwa kazi yenu hiyo

Muonayo niyapendayo

3.5 Choyo na husuda

Choyo ni ubahili na roho mbaya dhidi ya mwingine, na husuda ni kijicho kinachomfanya mtu amwonee gere mwenzake. Hali hizi hujitokeza katika jamii na husababisha migogoro na mitafaruku.

Sura ya nne : hitimisho, matokeo na mapendekezo

4.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho la jumla kuhusu dhamira na sababu za kutungwa kwa nyimbo za huzuni katika muziki wa taarab, hususan nyimbo zilizoimbwa na Fatma Issa, pamoja na mapendekezo yanayolenga watafiti wengine, wasanii na jamii kwa ujumla.

4.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza dhamira za nyimbo za huzuni katika taarab na sababu zinazowasukuma wasanii kutunga nyimbo hizo, kwa kutumia nyimbo za Fatma Issa kama kielelezo. Kutokana na uchambuzi uliofanywa, imebainika kuwa nyimbo za huzuni hazitungwi kwa bahati mbaya bali hutokana na matukio halisi yanayowakumba wasanii au jamii inayowazunguka.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa sababu kuu zinazopelekea kutungwa kwa nyimbo za huzuni ni pamoja na usaliti wa kimapenzi, migogoro ya kifamilia, msiba, choyo na husuda, fitina na uchongezi, majuto pamoja na hali ya kukosa bahati katika maisha. Sababu hizi zote zimebainishwa waziwazi katika nyimbo mbalimbali za Fatma Issa kama vile Nenda Utakako, Haya Maumbile Yangu, Asokasoro Hakuna na Fitina.Aidha, utafiti umebaini kuwa nyimbo za huzuni hubeba dhamira nzito zinazogusa maisha halisi ya mwanadamu. Dhamira hizo ni pamoja na kuelimisha jamii, kuonya dhidi ya maovu, kutoa maliwazo na faraja, kuizindua jamii kuhusu vitendo visivyofaa, pamoja na kuhimiza marekebisho ya tabia. Hivyo, nyimbo za huzuni si za kuburudisha tu bali ni chombo muhimu cha kijamii na kielimu.

4.2 Hitimisho la jumla

Kwa kuzingatia malengo ya utafiti na matokeo yaliyopatikana, inaweza kuhitimishwa kuwa nyimbo za huzuni ni sehemu muhimu ya muziki wa

taarab na zina mchango mkubwa katika jamii ya Waswahili. Kinyume na dhana iliyozoeleka kuwa taarab ni muziki wa furaha na ramsa pekee, utafiti huu umebainisha kuwa taarab pia ni jukwaa la kueleza majonzi, simanzi na masaibu yanayowakumba wanadamu katika maisha yao ya kila siku.

Imebainika kuwa wasanii hutumia nyimbo za huzuni kama njia ya kutoa hisia zao binafsi, kuwasilisha kilio cha ndani na kuakisi hali halisi ya jamii. Kwa muktadha huo, nyimbo za huzuni huendana kikamilifu na nadharia ya uhalisia ambayo inaeleza matukio kama yalivyo bila kupamba wala kuficha ukweli.

Hivyo basi, nyimbo za huzuni katika taarab hazipaswi kudharauliwa au kuchukuliwa kama kinyume na malengo ya asili ya taarab, bali zinapaswa kutambuliwa kama sehemu ya mageuzi ya sanaa hii kulingana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisaikolojia yanayowakumba wanadamu.

4.3 Mapendekezo ya utafiti

Kutokana na matokeo na hitimisho la utafiti huu, mapendekezo yafuatayo yanatolewa:

a) Watafiti wengine wahamasishwe kufanya tafiti zaidi kuhusu nyimbo za huzuni katika taarab kwa kutumia waimbaji wengine kama vile Shakila, Bi Kidude na makundi mbalimbali ya taarab.

b) Tafiti zijazo zijikite pia katika kulinganisha nyimbo za huzuni na nyimbo za furaha katika taarab ili kubaini tofauti za kimaudhui, kifani na kijamii.

c) Wasanii wa taarab wahimizwe kuendelea kutunga nyimbo zinazogusa hali halisi ya maisha ya jamii bila kuogopa kukiuka dhana potofu kuwa taarab ni ya furaha pekee.

d) Vyuo na taasisi za elimu viingize nyimbo za huzuni katika mtaala wa fasihi simulizi ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa mchango wa sanaa katika kuakisi uhalisia wa jamii.

4.4 Hitimisho la mwisho

Kwa ujumla, utafiti huu umeonesha kuwa nyimbo za huzuni katika taarab ni kioo cha maisha ya mwanadamu. Nyimbo hizi zinaakisi maumivu, majuto,

simanzi na mapambano ya kila siku yanayowakumba wanajamii. Kupitia nyimbo hizi, jamii hupata faraja, mafunzo na msukumo wa kurekebisha mienendo yao.

Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa nyimbo za huzuni zina nafasi kubwa katika muziki wa taarab na haziwezi kutenganishwa na maisha ya jamii ya Waswahili. Sanaa ya taarab itaendelea kubeba furaha na huzuni kwa pamoja kwa kuwa yote mawili ni sehemu ya uhalisia wa maisha ya mwanadamu

■Marejeo / References

1. Abdulaziz, M. H., & Nurse, D. (2006). *A History of Swahili Literature*. London: East African Educational Publishers.
2. Mazrui, A., & Mazrui, A. (1995). *The Swahili: Idiom and Identity in East Africa*. London: Hurst & Company.
3. Hinnebusch, T. (1981). *Swahili Literature and the Oral Tradition*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
4. Fadda, S. (2014). «Contemporary Swahili Poetry and Its Social Context.» *Journal of African Cultural Studies*, 26(3), 291–307.
5. Nurse, D., & Hinnebusch, T. (1993). *Swahili and Sabaki: A Linguistic History*. Berkeley: University of California Press.
6. Mkude, D. (2001). *The Evolution of Swahili Prose*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.
7. Mohamed, K. (2010). «Swahili Drama: Between Tradition and Modernity.» *African Studies Review*, 53(2), 87–104.
8. Burton, R. F. (1990). *Swahili Stories and Legends: An Anthology*. London: Heinemann.
9. Nurse, D. (1985). *Swahili Poetry: Forms and Functions*. Nairobi: East African Publishing House.
10. Alamin, M. (2007). *Modern Swahili Literature: Trends and Themes*. Dar es Salaam: TUKI Press.
11. Kiango, M. (2012). “Oral Tradition in Swahili Narrative Literature.” *Journal of African Languages and Linguistics*, 33(1), 45–67.
12. Mohamed, A. (2003). *Swahili Fiction: Historical and Social Perspectives*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
13. Knappert, J. (1992). *Swahili Tales: Retold from the Original*. London: Heinemann.
14. Whiteley, W. H. (1969). *Swahili: The Rise of a National Language*. London:

Methuen & Co.

15. Chale, S. (2016). «Women Writers in Contemporary Swahili Literature.» *Research in African Literatures*, 47(2), 23–40.

16. Nyerere, J. K. (1974). *The Role of Kiswahili in African Education and Culture*. Dar es Salaam: Government Printer.

17. Mohamed, R. (2018). *Swahili Poetry and Social Commentary: A Critical Study*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam Press.

18. Askew, K. (2002). «Performance and Identity in Swahili Oral Literature.» *Africa*, 72(1), 1–23.

19. Haji, H. (2015). *Language and Literature in East African Societies*. Nairobi: East African Educational Publishers.

20. Mdee, H. (2011). «The Influence of Arabic on Swahili Literature.» *Journal of African Cultural Studies*, 23(2), 157–174.